

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA AFYA

### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAHADHARI NA KIFO CHA MTANZANIA MMOJA KWA UGONJWA WA EBOLA NCHINI UGANDA

01, Oktoba, 2022.

**Ndugu Wananchi**, Siku ya tarehe 20 Septemba, 2022, Wizara ya Afya ilipokea taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya wa Uganda, kupitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya mlipuko wa ugonjwa wa Ebola katika Wilaya ya Mubende na Wilaya zingine tatu nchini humo. Hadi kufikia tarehe 29 Septemba, 2022, **jumla ya wagonjwa 54 walithibitika kuwa na ugonjwa huo na vifo 25 vilikuwa vimetolewa taarifa**

**Ndugu wananchi**, Tarehe 28 Septemba, 2022 tulitoa tamko la kuhabarisha umma pamoja na kutoa tahadhari juu ya ugonjwa huu kwa wananchi ikiwemo hatua za kuchukua ili kujikinga. Tarehe 01 Oktoba, 2022, Wizara ya Afya imepokea taarifa toka Wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki ikitoa taarifa ya kifo cha **Dkt. Mohamed Ali Hafidh** aliyekuwa akisomea udaktari bingwa wa upasuaji nchini Uganda akitokea Tanzania.

**Ndugu Wananchi**, Bado tunaendelea kusesitiza kuwa, uwepo wa ugonjwa wa Ebola katika nchi jirani kunaiweka nchi yetu katika hatari kubwa ya kupata maambukizi kutokana na mwingiliano mkubwa wa shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi. Tunaomba kuwajulisha Wananchi kuwa ugonjwa huu haujaingia hapa nchini, hata hivyo, **tunawataka wananchi kuchukua tahadhari zote ili kuhakikisha ugonjwa huu hauingii nchini.**

Serikali inatoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu pamoja na watumishi wote wa afya nchini.

Imetolewa na;

A handwritten signature in green ink, appearing to read 'Ummy A. Mwalimu'.

Ummy A. Mwalimu (Mb)

**Waziri wa Afya**

A handwritten signature in green ink, appearing to read 'Nassoro Mazurui'.

Nassoro Mazurui

**Waziri wa Afya SMZ**